

Shairi lifuatalo liliandikwa na Malenga Hamidu Tambwe miaka kadha iliyopita likizungumzia umuhimu wa utunzi mzuri wa mashairi na nasaha za kimaisha

GAZETINI USITIE

1. Leo naanza kutunga, Edita nikwandikie,
Na bila hata kuvunga, nipange niyachambue,
Edita hao malenga, yao usiyafatie,
Gazetini usitie, guni zilizobanangwa.
2. Japo wawe ni nyakanga, hao usiwatambue,
Watunze walo wahenga, gazetini uwatie,
Hao anza kuwatenga, kamwe usiwatambue,
Gazetini usitie, guni zilizobanangwa.
3. Huto tujinga tujinga, tuache tujisifie,
Kwani bado ni tuchanga, tusitonijua mie,
Mimi haki ntatutwanga, la kufanya tusijue,
Gazetini usitie, guni zilizobanangwa.
4. Iko siku nitatanga, nyumbani nitufatie,
Huku nikipiga chenga, makofi nituzabue,
Nitukomeshe kutunga, pia kunitusi mie,
Gazetini usitie, guni zilizobanangwa.
5. Majina wanajipanga, ya kashifa kwetu sie,
Ili waanze kutunga, na lugha waichafue,
Hao ndugu si wahenga, ya kwao usifatie,
Gazetini usitie, guni zilizobanangwa.
6. Wanajiita nyakanga, hali mwalimu ni mie,
Mimi ni wao mganga, Edita unitambue,
Leo eti wanipinga, Edita ujionee,
Gazetini usitie, guni zilizobanangwa.
7. Ngurumo wanakuvunga, hayo yote utambue,
Mimi ntaenda wapunga, ujinga niwaondoe,
Kisha niwapake unga, akili iwarudie,
Gazetini usitie, guni zilizobanangwa.
8. Beti nane nimetunga, sitaki niendeleo,
Na tafadhali muhenga, kapuni usinitie,
Ikiwa nimebananga, kwenye kapu kazitie,
Gazetini usitie, guni zilizobanangwa.

Hamidu R. Tambwe (1967)